

COUNTY ASSEMBLY OF SAMBURU



THE HANSARD

Tuesday, 30th April, 2024

The Assembly met at the County Assembly Chambers at 2:30 pm

The Speaker, (Mr. Lenamarle Stephen), in Chair

PRAYER

PAPERS

The Speaker, (Mr. Lenamarle Stephen): Honorable Lenamparasio

MCA Loosuk Ward, (Mr. Lenamparasio Phelix): Thank you Hon. Speaker, I beg to table the County's budget estimates for the Year 2024/2025. Thank you Hon. Speaker.

The Speaker, (Mr. Lenamarle Stephen): I commit this budget estimates to all our sectorial committees.

STATEMENTS

Honorable members, it is notified that pursuant to standing order 45-1(C), the speaker has approved the following tentative request for statements,

Statement Number 05/2024 requested by Honorable Esther Lenolkulal to the Chairperson of the Committee on Agriculture and Livestock in regards to the tractors and seed distribution.

Specially Elected Member, (Hon. Lenamatiyio Silapia): Thank you Honorable Speaker, I stand to read the statement sort by Honorable Esther Lenolkulal, I know members may ask why I am doing so while She is here, it is because she has given me the permission to read on her behalf in English Honorable Speaker.

Pursuant to standing order 45 (C), I hereby request a statement from the chairperson of the Committee on Agriculture. Livestock, Veterinary and Fisheries, in regards to tractors and seed distribution for Samburu County residence farmer

Honorable Speaker, some parts of Samburu county are known for Agricultural activities where crops play a vital role in the livelihoods of the residence, it is essential that we understand how these activities impact the people of Samburu County as their well-being is intergratedly tied to the success of agriculture in the region.

The county tractors and seeds distribution in agricultural productivity areas has profound impacts on the economic developments of the County; including food security, income generation and overall quality of life for the residents. It is crucial that we obtain this information to access the effectiveness of our agricultural problems, and ensure that the needs of the County residents are being met in a sustainable and efficient manner.

In view of this, the chairperson should enquire into and report on:

1. a) The current condition of agricultural machineries, specifically Tractors.
b) Have there been any recent upgraded or new acquisition of farmer machineries to support the farming community.
c) How many tractors are currently available for use by the community, and what measures are in place to ensure the proper maintenance and its efficient management?
2. The County Government promised to plough hectares of land in areas affected by banditry, what progress has been made in fulfilling this commitment, and the criteria or the requirements for farmers to benefit from it.
3. What are the insights into the coordination between the County government and the Local farming community in implementing the Land Ploughing Initiative?
4. a) Have there been any challenges or success in the management and use of tractors for Agricultural operations.
b) How have these challenges been addressed and what improvements have been made.
5. What are the insights in the distribution of seeds and specific villages that have received the allocation in the wards?
6. a) How has the quantity of seeds been distributed been determined
b) Are there specifics or criteria used to ensure fair distribution among the farmers?
7. a) What is the current budget allocation for providing seeds to the farmers in agricultural production areas?
b) How are the farms for the seed's allocation being managed and distributed to ensure equitable access for all eligible farmers?

That is it Honorable Speaker, I would like to call upon Honorable Esther to elaborate in Kiswahili.

Specially Elected Member, (Hon. Lenolkulkal Esther): Asante Mheshimiwa Spika,

nafikiri kuwa wale ambao hawajasoma wana nafasi ya kuongea, kwa sababu unaweza kuwa na maneno akilini na pengine hujui kuangalia karatasi hii, ningependa kuchukua nafasi hii

kumshukuru Mheshimiwa Silapia kwa kusimama na mimi na kunisomea, Asanti. Kwa kweli, mahali ambapo mimi nimetoka ni mahali ya ukulima, na imepita misimu miwili kwa sasa bila kuwa na trekta hizi za kaunti. Ningetaka kujua haswa kwani hapa Poro tulikuwa na vijiji vinne vilivyokuwa na trekta, ila tangia Mwaka wa 2022, matrekta haya hayajakuwa pale tena, hivyo ningetaka kujua matrekta haya yamerudi kuwa za kazi gani kiasi ya wakulima kule nitokako kulazimika kutumia trekta za kibinafsi zilizotoka Nyahururu ilhali matrekta ya kaunti yako hapa, yalirudishwa kwa njia gani ?, yanafanya nini?, yanasaidia nini?, ningetaka kujua kuhusu mambo hayo.

Jambo lingine Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwa sasa kuhusu suala la utovu wa Usalama, tulisikia serikali ikiahidi kusaidia wale watu ambao walilazimika kutoka makwao, waliahidiwa kuwa kila mmoja wao atalimiwa shamba hekari moja na vilevile kupewa mbegu ya kutosha hekari hiyo, lakini kufikia sasa hivi na hata hivi majuzi nikifuatilia trekta moja iliyokuwa ya Kijiji ya Lporokwai iliyotumwa kule Soit pus ikalime kule hata bila wenyeji wa shamba kuwa pale, ilikuwa ikiingia na kulima mahali na nilipowauliza kuhusu mbegu, walijibu kuwa hawakupewa na wakati huo pia walikuwa wakulima nusu hekari na kutoka, kufikia sasa hivi Mheshimiwa Spika ambapo mvua inaelekea kuisha, wengi ambao walibahatika kupanda kwa wakati wanapalilia mashamba yao, wale watu ambao waliahidiwa kulimiwa shamba yao na hata kupewa mbegu, wataweza kulima mashamba yao lini , watapanda lini na iwapo wataweza kupata mvua.

Lingine kwa kweli Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi hupenda kuongea ukweli hata mambo ikiwa vingine, kwa sababu wanaoumia sana na kina mama na Watoto, kwa upande wa wakulima, watu hawa huwa hawana ng'ombe wala mbuzi wengi, wao hutegemea mashamba yao kwa ajili ya kula, kulipa karo na hivyo nahisi uchungu sana kuwa watu hawa wapo misituni wakitaraji ahadi yao itimizwe kwa kulimiwa hekari moja, tunafahamu kuwa hekari moja kwa kawaida huchukua Kilo Kumi ya aidha mahindi na maharagwe, hivyo watapata lini, waweze kulima lini na kufikia lini watakuwa wamesaidika kwa mpango iliyosemekana. Hivyo singeweza kunyamaza na kuangalia watu wetu wakiumia na ingali walikuwa wameahidiwa jambo. Ningependa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo atueleze ni lini watu hawa watasaidika, kwa sababu muda unasonga. Asante Mheshimiwa Spika.

MCA Nachola Ward, (Mr. Lorunyei Lawrence): Asante sana Mheshimiwa Spika, Ningependa kumshukuru Mheshimiwa Esther kwa kuuliza mambo yaliyokuwa kwenye Kauli yake. Unajua kuwa kabla ya kupata uhuru, tulikuwa tukipigana dhidi ya mambo matatu; Ujinga, Njaa na Magonjwa. Ni aibu kufikia sasa kuwa bado tunazungumzia suala la njaa, na katika ugatuzi ambayo maana yake ni kupeleka huduma karibu na wananchi, ndiposa trekta zilinunuliwa ili badala yao kukomboa matrekta, serikali huwaletea matrekta haya karibu nao ili wananchi wapate kuyafikia kwa urahisi, inashangaza kwamba matrekta yanaulizana yalipo na pia huduma yao huku tunasema kuwa tunapigana dhidi ya njaa, mojawapo kati ya mambo tuliyosema kuwa tunapigana dhidi wakati wa uhuru.

Ninashangaa Zaidi kwani suala hili ni la dharura kwa sababu najua chakula pamoja na maji ni haki ya msingi,. Na ikiwa ni hivyo na hatuwapi wananchi wetu, basi kuna shida mahali na ninaomba Mheshimiwa Spika uangalie suala hili kwa uzito ili lijibiwe kwa haraka na tuone ni hatua gani tunaweza kuchukua kwa sababu hii ni mchezo mkubwa sana. Asante Mheshimiwa Spika.

MCA Poro Ward, (Hon. Leerte Patrick): Asante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii, ningependa kutia uzito kwenye usemi wa Mheshimiwa Esther kwa sababu unakumbuka wakati tulikuwa tukiulizia maneno ya ndume wale, niliulizia swala hilo la mbegu kwamba tunataka mbegu kabla ya Mvua kuja na pia matrekta yaweze kufika kuwalimia watu, la kushangaza ni kuwa kama alivyosema Mheshimiwa Esther, matrekta hayo yalikuja na yalienda kulima mashamba ambayo watu hawakuwa na yalilima mashamba, bila kuogopa niliona kuwa zilikuwa zikipielekwa matrekta mbili sehemu moja ilhali kuna sehemu zilizobakia bila, niliweza kumwuliza C.O na alinieleza kuwa ilikuwa ni amri ya Gavana.

Kwa hivyo, tukitumia mtindo huo hata wakati mwingine trekta huenda mahali ambapo watu wanajulikana na itakuwa ni ngumu kwa wengine. Aliyepeana trekta ndiye pia aliyewapa watu ahadi na watu walikaa wakingoja watimiziwe, Mvua imenyesha kwa sasa na hivyo mtu kupata trekta na kupeleka kuingia kulima huwa ni ngumu, kwa sababu mahali tumetoka huko Poro ambapo mvua ikinyesha zaidi ya wiki moja, huwa ni ngumu kulima.

Pili ni kuhusu mbegu, kama ambavyo huwa tunafahamu kuwa hekari moja huchukua kilo kumi na mbegu tulizoahidiwa kupewa ilitarajiwa kuwa ya kutosha, mbegu tulizopewa hata hivyo kwani nilikuwepo wakizipeana, walipeana kilo mbili kwa mtu mmoja. Hivyo ahadi iliyooleanwa

na serikali wakati wa mkutano , iliwazuia watu kujinunulia mbegu na hata kujilimia mashamba.Kulima na kununua mbegu kwa wakati ilizuiliwa na ahadi waliyopewa, sasa hivi waliamua kujilimia kwa sababu ya mvua kuisha, ukosefu wa trekta na mbegu.

Hivyo Mheshimiwa Spika tungependa Mwenyekiti wa kamati ya Kilimo atupe majibu hayo, kwani matrekta zilipopelekwa kule, zilifanya kazi kwa kupendelea watu wanaowajua ilhali wengine walipata matrekta hayo baada ya kumaliza kazi mahali pengine. Na hilo ni suala ambalo lipo na tuna Ushahidi wa kutosha kuhusu hili, kwani matrekta yalikuwa yakilima mahali na kupita mashamba mengine hata ingawaje wenyeji walikuwa na pesa, yaliendelea kupita tu na kueleza watu kuwa yatakuja tu. Kufikia sasa matrekta yanasimama wiki mzima kwa sababu ya kukosa mafuta, hata tukienda sasa hivi tutapata tu yakiwa yamesimama kwa sababu hiyo ya kukosa mafuta.

Ningependa kuelezwa sababu ya kutokuwepo kwa mafuta kwenye idara hii, kwa nini hakuna bajeti iliyotengwa kwa ajili ya mafuta ya matrekta na mbegu ilhali kulikuwepo na ndume zilizoununuliwa takriban mia tisa. Wale ambao waliweza kupata ngombe na ngamia ndio ambao walifaidi na kwa upande mwingine sisi ambao tuliahidiwa kulimiwa na kupewa mbegu tumepata hasara kwani hatujalimiwa mashamba na hatukupata mbegu ya kutosha. Mheshimiwa Spika, tunahitaji majibu hayo kwa haraka. Asante.

ningependa tu kushukuru mheshimwa spika kwa kunipa nafasi pia mimi nichangie. Langu tu ni kwamba ningependa kutia motisha mheshimiwa Esther na asijiskie kwamba ni udhaifu ama labda kuna kasoro usipokuwa labda na elimu ya Kiingereza manake nyumba hii tuko sawa na uko na nafasi kama tu wale wengine kunena yale ambaye inastahili hivyo bila shaka sio tu nyumba hii kulingana na sheria ama ratiba ambaye zimewekwa kanuni ni kwamba tunaweza zungumza Kiswahili, Kiingereza na hata lile lugha ya ishara.

Hiyo yote imekubalika kwa hivyo mheshimiwa usijiskie kwamba ni duni wewe ni mmoja wetu na uko na haki ya kunena na kuleta maneno kama haya ambayo yako mbele yetu na ni ya muhimu sana hasa kwa wananchi wetu ambaye ni wakulima ambaye wanastahili pia kupewa huduma kama namna vile ishaapangwa hio ndio ya muhimu kwangu.

Hii ingine sasa ya mambo ratiba na mambo ya tuseme ahadi na mpangilio mimi tu ningesema kwamba kuna taratibu na kulingana na kanuni ya nyumba hii nambari 87 inasema kwamba

wakati tunaponena na kutoa wajibu ama pendekezo ni lazima yawe sahihi na bayana wazi kulingana na sheria hivyo ni muhimu sana kwamba tuzingatie sheria tunapochangia mjadala kwamba kanuni za nyumba hii lazima ifuatwe hasa hizo. Nadhani kwa ruhusa yako Bwana Spika japo hatupendi kuchanganya. *Standing order number 87 calls for facts of statement.*

Hio tu ndio nilikuwa nataka kusema mwenyekiti ako na haki ya kutuelekeza na kwa sababu yeye sio wale ambaye wanatoa huduma yeye pia atanena zake ambaye anajua lakini ni mzuri sana kwamba ameweza kusema kuna shida na shida hilo wacha ifuatiliwe na mwenyekiti na tupatiwe suluhu ama wajibu sahihi. Asanti Bwana Spika.

Asanti sana mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mimi kabla hata niendeleo ningetaka tu kumpongeza mheshimiwa Esther kwa pendekezo hilo la hio kauli, mimi kama mwenyekiti wa kamati nataka kukubaliana na wewe kwamba kuna shida na mimi vile mheshimiwa Lemoosa amesema hapa mimi ni kuleta habari kutoka upande ule wa Executive na nitahakikisha ya kwamba nitaleta hio habari kwa haraka iwezakanavyo.

Ni mzuri tu tujue ya kwamba tunaenda kwa pumziko ndogo recess hivyo mi nataka tu kuambia mheshimiwa Esther na waheshimiwa wengine siku ile tutarudi nitahakikisha kwamba hio ripoti iko hapa na nitaleta ripoti ya ukweli na ya haki hivyo mi nakubaliana kabisa na Esther na nitahakikisha ya kwamba nitafuatilia hio maneno tukirudi nitakuwa nimeleta hio majibu kwa hii nyumba. Asanti sana Bwana Spika.

Asanti sana mheshimiwa Spika na mheshimiwa spika sikuwa nimeweka tarehe kwa sababu sikua najua tutarudi kutoka recess tarehe gani. Mheshimiwa Esther tarehe nne mwezi wa sita, saa nane na nusu nitakuletea majibu yako hapa. Asanti sana.

MCA Nyiro Ward, (Hon. Lemoosa Jonathan); Asanti sana Spika. Ijapo sio kanuni kunena baada ya uamuzi wako na mwelekezi mimi tu ningependa pengine kusema hivi, mwenyekiti amesema vizuri lakini kulingana na yale mheshimiwa amesema ni hali ya dharura hivyo pengine kama kamati wangeweza tu kupeleleza na kuweza kumwelekeza ama kumpa suluhu yale ambaye yanahitajika kufanyika ili wale wananchi wafaidike sio tu labda kazi ziendeleo mpaka tarehe hiyo.

Najua mwenyekiti ni mtu ambaye ana bidii na ni mzuri sana tuzingatie hizi kwa haraka na kwa pupa ili wananchi wahudumiwe. Naomba tu msamaha bwana spika kwa sababu sio kanuni ya

nyumba hii kunena baada ya wewe kupatia mwelekeo lakini naona tu kwa sababu ya umuhimu yalishughulikiwe lakini tupate arifa hapo baadae. Asanti.

Mheshimiwa Spika, asanti sana Mheshimiwa Lemoosa nataka tu kusema hapa naomba tu hii nyumba inipee ruhusa alhamisi tukikuja hapa saa nane hata si kujibu hio kauli lakini ile vitu ya dharura nitajaribu kufuatilia kwa upande ile ya idara ndio nilete habari hata kama sio kujibu hilo kauli.

Lakini ile habari ya dharura kama hio ya mafuta ya matrakta nitahakikisha ya kwamba leo na kesho hata kama itakuwa ni likizo nitafuatilia kwa simu alhamisi asubuhi nitakuja niende huko kwa idara nifuatilie kwa hivyo saa nane nitaleta tu habari lakini si kujibu kauli lakini kuna habari nitakupea ya muhimu kwa sababu hatutaki kazi isimame. Mwezi mzima kwa ukulima ni muda kubwa sana kupoteza hivyo asanti sana mheshimiwa spika

The Speaker, (Mr. Lenamarle Stephen); Statement Number 06/2024 requested by honorable Esther Lenolkulal to the chairperson of the committee on medical services, public health and sanitation in regards to the status of Poro Health Centre. Honorable Silapia

Specially Elected Member, (Hon. Lenamatiyio Silapia); Thank you, Hon. Speaker. I still stand to read for the Esther statement so allow me to read. Honorable Speaker pass one to standing order 45C I hereby request for a statement from the chairperson of the committee on the medical services, public health and sanitation in regards to status of Poro Health Centre. Honorable Speaker, the Constitution of Kenya 2010 entails every person has right to the health care services chapter four on the bill of rights states in article 43/1 that every person has the right the highest attainable standard of health which include the right to health care services include reproductive health care and that person shall not be denied emergency medical treatment. Honorable Speaker in view of this the chairperson should inquire into and report on;

1. A) What is the current status of electricity supply at Poro Health Centre?
1. B) What measure that are being taken to address the lack of electricity in Poro Health Centre?
2. A) What is the current status of the employment of the casual staffs at the Health Centre?

B) What are the payment steeped for subordinate staffs in place to ensure fair compensation and support?

Thank you Mr. Speaker I call upon Hon. Esther to explain her statement in Kiswahili, Thank you.

Specially Elected Member, (Hon. Lenolkulal Esther): Bwana Spika naomba radhi kwa sababu pengine watu wanadhani leo bunge ni yangu pekee, wasamburu wanasema kwamba wakati wa kuongea ikifika kama hauna maneno ya kutamka hautaongea ilihali ukiwa na maneno ni lazima uongee, na kwa kweli maswala ya Poro ni kama imekuwa ngumu kidogo.

Kwa sasa Poro stima ilikatwa, kuna ukosefu wa usalama na zaidi ya hayo jusi kulikuwa na mjamzito saa nane ya usiku alikuwa anajifungua na kwa sababu Poro hakuna stima ilibidi aletwe Maralal na pia hatuna gari lolote, hatuna ambulansi wala mbinu yeyote ya kumsaidia, na ilikuwa shida kwangu kupigiwa simu usiku wa manane kwenda kumchukua mama huyo kumlete Maralal na pia siku hiyo sikuwa na dereva nyumbani ilibidi nitafta mbinu nyingenezo afikishwe hospitalini kwa kweli niliskia uchungu sana mheshimiwa, naona haya sana kulalamikia ukosefu wa stima kwa sababu ya bili kidogo sana, hili swala linatuumia sana kama wamama.

Swala lingine ni, kwa sasa watu hawapati matibabu kwa sababu hakuna pahali pa kuweka dawa, wamama waliojifungua hivi majuzi wanaenda Seketet kutafutia watoto wao chanjo kwa zahanati na tunajua kuna ukosefu wa usalama pamoja na mvua, ningeomba kufahamu kwamba nini inayoendelea? kama Poro haiko kwa hesabu tuambiwe ndo tujipange tuwe tukibeba wamama wetu kuleta hospitali tukijua hakuna hospitali Poro. Bwana Spika katika eneo hilo mimi ndiye naishi upande wa mwisho na ninahatarisha maisha yangu nikitoka kwangu kuelekea hicho kituo kuchukua mama huyo na kumtafutia gari aletwe hadi Maralal ili aje ajifungue saa kumi na moja asubuhi. Hili ndilo swala lililonifanya nije kuongea hapa Bwana Spika.

Swala lingine Bwana Spika ni wale watu wanaofanya kazi ya mikono (Casuals) ama sijui nini imeandikwa hapo, kesho yake nikienda hapo kuulizana maneno ya hiyo hospitali hawa watu wanafanya kazi hapo, imefika saa hizi miezi nane bila kulipwa na nikiuliza wanalipwa pesa ngapi wakasema ni elfu nne mia tano mwengine elfu nne hadi mlinzi akatoroka kwa sababu ya ukosefu wa pesa kwa hivyo swala hili ni la dharura tena zaidi kwa sababu ata afadhali shamba

likae bila kulimwa juu naweza lima shamba kesho yake ilhali mama mjamzito hawezi kuhahirishwa hadi siku nyingine akijifungua.

kwa hivyo hii maneno hatuoni kubwa sana na sijui sisi tuko dunia gani ndio basi tujipange wamama warudi kujifungua kule manyumbani kama ni hiyo, tuko na mama mwengine mmoja ambaye anasaidia hawa wamama bali hajaajiriwa na amekuwa akifanya kazi hapo miaka kumi na tano ningeomba Mheshimiwa mwenye kiti arejeelee maswala hayo ya poro kwa sababu tunaumia sana; ukosefu wa usalama, hatujalimiwa mashamba ,wamama wanajifungua njiani, hakuna stima, kwani tuko nchi gani hapa? Nashukuru Bwana Spika.

MCA Elbarta Ward, (Hon. Leitoro Jeremiah): Asante sana Mheshimiwa Spika napenda kuchukua fursa huu kushukuru mwenzangu Mheshimiwa Esther Lenolkulal kwa kuleta hoja hii kwenye hiki kikao, swala la mstima ni muhimu sana Mheshimiwa Spika panapofikia mahali stima hakua kwenye vituo vya afya kazi pia inakuwa nguma sana Mheshimiwa Spika.

Ningeomba muda ya wiki mbili ilihali sina ratiba kamili yah hii nyumba yetu nimeskia likizo kidogo ndiposa naomba mwelekeo wa siku ambayo ningependa na ningependa kuchukua fursa fupi sana na sijui tarehe kumi na nne mwezi wa tano itakuwa siku basi jinsi alivyo Mheshimiwa Lenamparasio alitangaza maneno kwa sababu ili ni jambo la dharura mimi ngeomba fursa huu kufuatilia, tuingoja kuleta jibu kamili kulingana na usemi uliosema ma mheshimiwa Esther Lenolkulal, tutafuatilia hili kujua shida ilikuwa nini na kama inawezakana jawabu tupate kabla hiyo siku ambayo usemi rasmi inaletwa mweheshimwa spika hilo ndilo jambo ambalo ningependa kufuatilia, inaonyesha kwamba shida ya stima si pekee kwenye vituo vya afya ilhali pia hapa penye tuko ndiposa ningependa kuuliza hilo swali ya nini ndo inafanyika huku?

Hapa tunan'gan'gana sana kwa kufanya kazi ya mikono, ili jumba halipaswi kukosa stima, nafikisha hapo mweheshimwa spika utanipea fursa ya kupanga tarehe kamili ya kurudisha hilo jawabu.

MCA Nyiro Ward,(Hon. Lemoosa Jonathan): Nashukuru mheshimiwa Spika kwa fursa hii, naunga mheshimiwa Esther Mkono kwa swala hili la wafanyakazi kwenye mazahanati ama Hospitalini zetu kwa mfano hospitali ya South Horr, Tuum na Wuas Rongai vilevile kwa shida hiyo ya malipo mwenyekiti ningeomba kwenye hali ya ufasaha na malipo, ningeomba watu wangu wa Nyiro Ward wauganishwe , hawajalipwa na wamejaribu mwezi tisa hawajalipwa,

mwenyekiti aangalie ni nini inafanyika kwa sababu kidogo inatia hofu na pia ni huruma hawa ni wazazi wa mahitaji mbalimbali, mwezi tisa bila kulipa inaleta mshtuko, Asante Bwana Spika.

MCA Nachola Ward, (Hon. Lawrence Lorunyei): Nashukuru sana mheshimiwa Spika kwa fursa hii kwa maoni ya mheshimiwa Esther lakini nashangaa kama Gatundu, othaya, na kabarak ambayo kama sasa poro Gatundu wa Samburu county inalia na je Nachola sasa na sehemu zingine? inaonekana mashida ziko kwenye hospitali zetu zote mngejumuisha kuangalia kwa jumla kila Ward swala hilo ndiyo nilitaka kuongeza kwa mwenyekiti aangalie kwa sababu Kabarak, Gatundu na Othaya wa Samburu wakilia je? Nachola italia namna gani?

Specially Elected Member, (Hon. Lenamatiyio Silapia): Thank you Mr. Speaker, I would also like to shade light on the same, we are experiencing a lot of challenges as Samburu County on the issue of health services. Even me coming from Wamba North ward, we have some dispensaries that had been constructed, they have employed nurses, but those nurses are not available, the drugs are not there, so I do not know what is not happening.

I just want the Honorable Chair to enquire also as we have a dispensary at Sirata Lemurit in Wamba North Ward that we had allocated a budget in 2022/23 Financial Year, at least they have done something but up to today it is not completed. So, we wanted to know the status of that dispensary so it is just my request that the Honorable Chair would enquire on the same since we have these issues. I think honorable speaker you will give the directives on how the chair will go and collect about this sensitive matter. Thank you Honorable Speaker.

MCA Suguta Ward, (Hon. Leleruk James): Asante sana Mheshimiwa Spika, ningependa kumshukuru Mheshimiwa Esther kwa kuleta wazo kama hili, Kwa kweli Samburu kwa ujumla na sio kwa kawaida kwani Mwenyekiti anaweza kusema kuwa yale ambayo ameulizwa ndio anaweza fanya, kuna shida kwa upande wa Afya na shida kama hii ni sisi kama wawakilishi wadi ndio tunaweza saidia kwa sababu kama kuna uti wa mgongo wa Kaunti ya Samburu basi ni hospitali.

Iwapo Hospitali haitakuwa na wafanyikazi na dawa, au hata watu wa kufanya kazi na kulipwa basi itakuwa ni shida. Nimesikia Mheshimiwa Esther akilalamikia kuhusu wadi yake kuachwa, si hivyo, takriban wadi zote ziko hivyo na ni kwa sababu ya mambo yanayohusu rasilimali. Lakini ninataka kusema hivi, tukiwa kwenye chumba hiki, ninawasihi sana kuwa tutoe amri kwa

msimamizi wa hospitali aangazie kwa kina na afanye uchunguzi mzuri kuhusu ripoti atakayowasilisha mbele ya chumba hiki. Najua waheshimiwa watauliza maswali mengi, kuuliza ni suala moja ambayo itazua mengi.

Kwa hivyo ninaomba, sisi kama wawakilishi wadi kuwa kweli tumeona shida ilipo na najua kuwa kwa bajeti tuliyotengeneza hivi juzi, mambo yanayohusu maji, afya, barabara ni masuala tunayofaa kuzingatia na kufahamu pale ambapo shida ipo kama waheshimiwa kwani ndizo misingi ya maendeleo. Namuunga Mheshimiwa Esther mkono kwa hili na namsihi Mwenyekiti wetu kwani najua anaweza, atuwasilishie ripoti kamili. Afanye ripoti ya jumla ya wadi zote kwani kila wadi tuna jumbe nyingi ya watu kutolipwa kwa miezi nyingi, wengine wao kufanya kazi kwa miezi kumi na miwili na hata kumi bila kuandikwa, baada ya serikali mpya kuingia kuna wengine walihisi wapo maegeshoni baada ya watu wengine kuletwa, hivyo tuangalie masuala kama hayo. Asante Mheshimiwa Spika.

The Speaker, (Mr. Lenamarle Stephen): Hivyo mwenyekiti atuletee jibu kwa sababu tutarudi kutoka mapumziko baada ya Mwezi moja, na suala kama vile la stima kukatwa haiwezi ngoja Mwezi moja, hivyo ajaribu kama vile yule wa Kilimo alivyofanya ikiwa ataweza kutupa majibu Alhamisi ya hii wiki Saa nane, lakini ripoti kamili atawasilisha Tarehe Nne mwezi wa Sita. Lakini ajaribu leo au Kesho kuongea na wahusika ili mambo ya usambazaji wa stima tuweze kupata jibu Alhamisi hii Saa nane unusu. Asante sana. Natumai hilo liko sawa.

Honorable Members it is notified **THAT** the following statements are due for response today being Tuesday 30th 2024 at 2.30 PM pursuant to Standing Order 45(C);

Statement No. 027/2024 requested by Hon. Jeremiah Leitoro to the Chairperson of the Committee on Finance, Economic Planning and ICT in regards to the departments Health's budget for the financial year 2024/25. Chairman Finance, Honorable Minority Leader.

MCA Suguta Ward, (Hon. Leleruk James): Mr. Speaker I rise as the defender of the government, I have seen that the chair and the vice chair for finance are not within and also I have not received any statement concerning the same. So, we are asking for Thursday 2.30 PM. Thank you Mr. Speaker.

Thank you Honorable Speaker, I think it is so unfortunate that today I stand in this house expecting to get the answers for the reason as to why the ceilings for the department of Health

was reduced from 1.6B to 1.4B. And now considering the emerging issues as we have observed already, it is just too much.

The budget that had been allocated Honorable Speaker, the 1.4B that is totals both development and the current. Keeping in mind that almost 1.3B goes for salaries which when we subtract from it, we will be remaining with 100 Million. So, what we usually require for drugs is 160 Million, and the balance was only 100 Million. Bills for Electricity is 30 Million annually and we have not talked about Stipends for CSV's which usually amounts to 48 Million, about fuel and repair of ambulances,

Whoever understands that's county strategic fiscal paper usually whatever amount has been adopted last week we adopted with a recommendation latter the CEC finance should actually increase the ceiling from 1.4 to 1.2 to retain the original 1.6B so that the service especially department of health will not be disorganized in many ways honorable speaker and not sure if the recommendation we have given here will be implemented, and now that there is no any answer that was given I stand here honorable speaker this how we are not giving the priority to important department like the department of health.

Honorable speaker and in that regard I even thought we are supposed to have receive the budget, to have table today the budgets estimates and if the budgets testaments thus with original that is 1.4M then i think honorable speaker we need to prepare our honorable members psychologically that we should be ready and prepared because majority of hospitals should be closed and that is facts that's how serious things are honorable speaker, there is departments that are really sensitive honorable speaker and I do not know am going to tackle this issues honorable speaker maybe through your guidance.

I will get the response today then before we see or before we table the budget testaments honorable speaker at least the budget ceiling for the department should have maintain the 1.6 because initially the request that was there was to increase 1.6B to 1.8B then instead of ceilings increasing to 1.8B the ceilings has been decreasing by 200M to 1.4, so am really dissatisfied and I don't know with the direction of honorable members which direction are we heading as county and honorable members and it could be painful if I will be up and part and parcel of the team and instead of impressing the services of the department of health I will be the part that really reduces the budget for the department, Thank you honorable speaker.

The Speaker, (Mr. Lenamarle Stephen): Honorable majority leader as a defender of county government as we said I don't know if we have a member of the finance committee here? now what we need to do is because last week the statement was issued last week and we are supposed to get the response today and we don't have the response and I think it is urgent therefore honorable majority leader and your team we need to have the response on Thursday on 2.30pm if you don't get the response on Thursday we assume the department and the committee is not working so let us have a comprehensive response on Thursday about the same, Hon. Silapia

Specially Elected Leader, (Hon. Lenamatiyo Silapia): Thank you honorable speaker I think we need to give honorable member to formulate on the same because I do remember am the one who read that statement and we requested the member of the committee lead by the chair to respond on this same day looking in the mood of the members who are sitting on that committee it seems that they are not even aware so even that day I asked you to give us the direction and also to assist the committee to get the response because this a sensitive matter and before we came to this respond we were discussing the concern that is affecting all the health sectors across Samburu county and honorable speaker this is the concern that has been going all around .

When you give out the statement keep on reminding the committee plus the departments and I don't blame the committee honorable speaker and I don't blame the committee I blame the department but also who were to be blame it is the committee members because were not serious honorable speaker and that why here we have no electricity when the session is going on therefore honorable speaker we need your guidance this is very serious matter, we look at the department of health being reduce again here we are discussing the challenges we are facing, you here the Poro Ward dispensary the have not paid fifty thousand for electricity and similarly you're seeing the budget of health being reduced.

The other day you heard us complaining about the swaari ambulance and even today when you talk about 100M in the department of health going to development then do you expect other ambulance honorable speaker? We need seriousness honorable members, we can't be here to say we are doing emphasis and representing the community, who are you representing if the whole North Wamba Ward has got no any ambulance for the last ten years? And other many issues honorable speaker just visit this near referral hospital you will get mothers from Wamba North Ward who were referred back from Wamba Ward to Maralal referral Hospital just because we

got no any theater in Wamba and because all the catholic hospitals have been already closed, So what can we do? Because that was the only theater hospital that was helping our people.

The other day we lost a mother just because she was giving birth to twins, and she gave birth to one kid and in that situation because there is no ambulance and no operation emergency that could be done at that particular time there we lost a mother with her child, it is so painful that we reduce the department of health and increase the land department, then what are we doing here honorable speaker?

We are protecting our lands so that our children could inherit, and we are going on losing our people that is what I can say, with your help honorable speaker and we have able chair and that day I said we that response on 30th before we table the estimate this is the estimate we have already tabled even the department of finance having no clue of the issue we are talking, honorable speaker we need to be serious here or else we close this assembly because we are doing nothing. Thank You.

The Speaker, (Mr. Lenamarle Stephen): We are not seeking responses and therefore honorable Silapia when you say you need guidance from the chair or from the speaker we only give guidance when we get the response and therefore if you are not going us the committee to the department and seek response then there is nothing you are going to do, so what we do I think I gave out the guidance on Thursday 2.30pm the minority leader and members give us the response here at 2.30pm then now if there is no response at 2.30pm, we can take another direction I think that is clear, Thank You.

ADJOURNMENT

Honorable Members, the time being 6.06 o'clock and there being no any other business this assembly adjourns till Thursday 23rd May 2024 at 2: 30 pm.